



NATIONAL  
**CERVICAL SCREENING**  
PROGRAM


A joint Australian, State and Territory Government Program

# Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi - chaguzi zako zimefafanuliwa

Kupata Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi kila miaka 5 kutasaidia uendelee kuwa na afya, kwa ajili yako na ya familia yako



1. Uchunguzi wa mlango wa uzazi ni mmoja wa njia bora kujikinga na kansa ya mlango wa uzazi - ili uweze **kuwa na afya kwa wewe na familia yako.**



2. Ni **kipimo kirahisi** unachoweza kupata **kila miaka 5** cha virusi viitwavyo HPV vinavyoweza kusababisha kansa ya mlango wa uzazi.




3. Ikiwa wewe ni mwanamke au mtu mwenye mlango wa uzazi, una umri kati ya miaka 25 na 74 unapaswa **kuzungumza na daktari wako au muuguzi** kuhusu kupata Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi.



4. Una **uchaguzi** jinsi ya kufanywa Kipimo chako cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi. Kuna chaguzi mbili na unaweza kuchagua ni ipi inayofaa kwako.



5. **Daktari wako au muuguzi anaweza kufanya kipimo kwa ajili yako.** Katika nafasi ya faragha, utaulizwa kuvua nguo zako kutoka chini ya kiuno na kulala chini ya shuka.



6. Daktari au muuguzi atachukua kipimo kutoka mlango wako wa uzazi. Inaweza utajikisia usumbufu kidogo hutasikia maumivu. Itachukua dakika chache tu.



7. Au unaweza **kukusanya kipimo wewe mwenyewe.** Daktari wako au muuguzi ataeleza jinsi ya kuchukua kipimo chako na akupe nafasi ya kibinafsi. Uliza daktari wako au muuguzi kukuonyesha mwongozo mwingine kama huu kukusaidia kukusanya kipimo chako yenyewe.



8. Chaguzi zote mbili ni njia za salama za kupata Kipimo cha Uchunguzi wa Mlango wa Uzazi. Kumbuka, unaweza kuuliza kuwa na daktari au muuguzi wa kike kama unapendelea.

**Panga miadi** kuzungumza daktari wako au muuguzi. Unaweza pia:

- tembelea [health.gov.au/NCSP-multicultural](https://www.health.gov.au/NCSP-multicultural) ili kupata taarifa zaidi kuhusu uchunguzi wa mlango wa uzazi
- piga simu kwa **1800 627 701**
- piga simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS Taifa) kwa **13 14 50** ili kupata msaada katika lugha yako.